# Makutano kati ya Dini ya Jadi na Dini za Kigeni: Mifano kutoka Riwaya Teule za Kiswahili

Lameck E. Mpalanzi
Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam

**Ikisiri**

Afrika ni bara la watu wanaoamini katika dini ya jadi ama dini za kigeni. Hata hivyo, kwa miongo mingi kumekuwa na tofauti za kiimani kati ya waumini wa dini ya jadi[1] na dini za kigeni, kila upande ukijiona uko sahihi kiimani na kimtazamo kuliko upande mwingine. Hali hii imesababisha migongano ya kiitikadi, kinafsia na kijamii. Makala hii inatetea hoja kwamba pamoja na kuwapo kwa migongano hiyo, dini za kigeni ni mwigo na mwendelezo wa misingi iliyowekwa na dini ya jadi ya Kiafrika. Katika kutimiza lengo hili, makala inaeleza dhana ya dini ya jadi na dini za kigeni, mitazamo ya kila dini na makutano ya dini hizo. Data kutoka riwaya teule za kiethnografia inashadidia kuwapo kwa makutano ya dini tajwa. Hoja za ulinganifu na makutano zinaangazia dhana ya kuwapo kwa Mungu, madhabahu, maleba na vifaa vya dini hizo. Hoja zingine zimezingatia malengo ya dini, watendaji wake na suala la utoaji sadaka. Pia, kuna ulinganifu kuhusu miiko, amri, sheria na mitazamo ya dini hizo kuhusu dhana ya maisha.

## 1.0 Utangulizi

Dini ni mfumo wa imani wa kuabudu na kuheshimu Muumba. Makundi makuu ya kidini yanayotambulika zaidi barani Afrika ni ya jadi na ya kigeni. Dini ya jadi hujumuisha imani na tajiriba za Waafrika zilizokuwapo tangu jadi na zinazodhihirika leo kwa Waafrika wengi. Ni dini inayotumika na kuongoza maisha ya Waafrika tangu jadi. Ijapokuwa dini hii haiko katika maandishi, bado inaongoza jamii kwa misingi ya usiri, mafumbo na ufunuo. Pia, dini hii huelezwa kupitia visasili, ngano, nyimbo, methali, misemo, vitendawili, litrujia na tambiko. Aidha, dini ya jadi huhifadhiwa na kuelezwa kupitia ishara, nembo, majina ya watu na

[1]Kumekuwa na mjadala mrefu kati ya wanaoamini kuwapo kwa dini moja ya Kiafrika (Awolalu, khj; Gathong, 2001; Ekeke na Ekeopara, 2010 na Antony, 2014) na wale wanaodai kuwapo kwa dini nyingi za Kiafrika (Magesa, 1997; Mbiti, 2011). Kwa mfano, Awolalu (khj) anaamini kuwapo kwa dini moja ya Kiafrika kwa sababu dini zote za Kiafrika zina ulinganifu wa kuabudu Mungu mkuu mmoja, miungu na utabiri. Kwa upande mwingine, Mbiti (khj) anadai kuwa tunazungumzia kuwapo kwa dini za Kiafrika katika uwingi kwa sababu kila jamii ya Kiafrika ina mifumo yake ya kuabudu... Hivyo, katika makala hii, tunakubaliana kuwapo kwa dini moja ya Kiafrika kwa sababu dini zote zina ulinganifu wa kuabudu, kuwapo kwa madhabahu maalumu, utoaji sadaka, kafara, utabiri na hata imani kuhusu kuwako.

mandhari takatifu (Awolalu, 1976). Kama zilivyo dini nyingine, inasemekana kuwa dini ya jadi iliibuka kutokana na tajiriba za kibinadamu na miujiza ya kiulimwengu. Katika kuipambanua miujiza hiyo, mwanadamu alijiuliza maswali mengi na hatimaye kubaini kwamba kuna nguvu mbalimbali za kiulimwengu zilizo juu yake. Kwa upande mwingine, dini za kigeni zitakazotolewa mifano katika makala hii ni Ukristo na Uislamu. Kwa mujibu wa Mbiti (2011), Ukristo ni dini inayoamini katika Yesu Kristo. Mbiti anafafanua zaidi kuwa Ukristo ulianzia Misri, na kufikia karne ya 7, takribani theluthi ya Waafrika walijiunga na kuamini katika Ukristo. Kwa upande mwingine, dini za kigeni ni zile zilizoingia kutoka nje ya bara la Afrika. Uislamu uliasisiwa na mtume Muhammad huko Arabia katika karne ya 7, na baada ya kifo cha Mtume huyo mwaka 632, wafuasi wake walianza kuueneza katika bara la Afrika. Sala ndiyo nguzo muhimu katika kuwasiliana na Mwenyezi Mungu na kuitakasa roho. Kufafanua dini hii, naye Mutiso (2015) anadai kuwa Waislamu hutarajiwa kusali mara tano[2] kila siku wakielekeza nyuso zao katika mji wa Makka.

## 2.0 Tajiriba ya Dini ya Jadi ya Kiafrika na Dini za Kigeni

Dini ya jadi huweza kutambuliwa pia kama dini asili (Awolalu, 1976; Gathogo, 2001; Gyadu na Otomoye, 2011). Wataalamu hawa wanafafanua kuwa dini ya jadi ni kongwe na ilikuwapo kabla ya dini nyingine kama Ukristo na Uislamu. Baada ya kuingia kwa Ukristo, waumini wa dini ya jadi waliitwa *wapagani* wakibezwa kuwa dini yao imefungamana na ushirikina. Aidha, baada ya kuingia kwa Uislamu, waumini wa dini ya jadi walibezwa zaidi kwa kuitwa *makafiri*. Katika kufafanua dini ya jadi, Awolalu (1976) anasema:

> ...tunapozungumzia dini ya jadi ya Kiafrika tunamaanisha imani na desturi ya dini asili ya Waafrika. Ni dini ambayo inatokana na kushikilia imani za mababu wa Waafrika wa leo, na inayoabudiwa nyakati hizi kwa namna na vivuli tofauti na uzito, na idadi kubwa ya Waafrika, wakiwamo wale wanaodai kuwa ni Waislamu au Wakristo... (Tafsiri yetu).

Maelezo haya yanashadidia kuwa dini ya jadi ni chimbuko la dini nyingine na imekuwa ikirithishwa kutoka kizazi na kizazi. Ama kwa hakika, pamoja na umuhimu wa dini hii kwa Waafrika, ujio wa wamisionari na wageni wengine uliathiri ukuaji wake. Awolalu (khj) anaeleza kuwa Wamisionari na wafuasi wao walidharau na kupotosha kuwa dini ya jadi ni duni, imejaa ushenzi, huabudu sanamu, imejaa ukafiri, uchawi na upagani. Hivyo, dhana ya upagani ilitumiwa na waumini wa dini za kigeni kama jitihada ya kushusha hadhi ya dini ya jadi. Kwa mtazamo wetu, hata huko Ulaya, lipo kundi la watu wasio wafuasi wa Ukristo au Uislamu lakini hawaitwi wapagani.

[2] Falsafa ya dini hii ipo katika sala tano: Alfajiri, adhuhuri, alasiri, magharibi na usiku. Pamoja na sala, nguzo nyingine zilizo msingi wa dini hii ni pamoja na kumwabudu Mtume Mohammad, kutoa zaka, kuhiji na kufunga Ramadhani.

### 3.0 Makutano ya Dini ya Jadi na Dini za Kigeni

Katika kukamilisha ulinganifu wa dini hizi, makala inatumia data kutoka riwaya za kiethnografia za Kiswahili. Riwaya zilizoteuliwa ni *Kurwa na Doto* (Farsy, 1960), *Mirathi ya Hatari* (Mung'ong'o, 1977) na *Bw. Myombekere na Bi. Bugonoka* (Kitereza, 1980). Hizi ni riwaya zinazohifadhi masuala muhimu ya kiutamaduni na jamii kwa ujumla. Uteuzi wa riwaya hizi umezingatia hoja kwamba mawazo yanayohusu dini yanajitokeza na kuingiliana kwa uwazi zaidi. Data hii inashadidiwa kwa maelezo ya watoataarifa kutoka katika maeneo ya Makunduchi, Njombe na Ukerewe. Riwaya hizi teule zinathibitisha kuwapo kwa makutano ya dini ya jadi na dini za kigeni, kama ifuatavyo:

### 3.1 Kuwapo kwa Mungu Mkuu na Majina yake

Waumini wa dini ya jadi wanatambua kuwapo kwa Mungu Mkuu. Kwa mujibu wa Mbiti (2011a), Mungu Mkuu anajulikana kwa majina mengi yanayoelezea tajiriba za Mungu. Baadhi ya majina hayo ni *Onyankopon* (Ghana), *Mulungu* (Kenya na Msumbiji), *Unkulunkulu* (Malawi, Zimbabwe na Afrika Kusini), *Molimo* (Lesotho), *umkhulumncand* (Swazilandi) na *Imana* (Burundi na Rwanda). Majina haya hubeba maana zinazoelezea asili, majukumu ama mahusiano ya Mungu na wanadamu. Kwa mfano, katika jamii ya Igbo nchini Nigeria, jina *Chineke* au *chukwuamon* lina maana ya nguvu iliyoumba vitu vyote, wakati majina kama *Nyadenga* na *Wakumusoro* katika jamii ya Washona wa Zimbabwe humaanisha Mungu anayetawala anga. Kimsingi, katika jamii za Kiafrika, majina yanayomtaja Mungu huashiria kuwa Mungu ni muumbaji, mlinzi, mtawala na mwasisi wa mipango yote. Aidha, majina mengine hufumbwa kisitiari kuashiria kuwa Mungu ni chanzo cha mithiolojia, tambiko na imani. Pamoja na kuwapo kwa Mungu Mkuu, maombi ya waumini wa dini ya jadi hupitia kwa miungu, mizimu na wahenga wanaoaminika kuwa karibu zaidi na jamii.

Aidha, kabla ya ujio wa wazungu, dini ya jadi ndiyo iliyotamalaki na kupewa kipaumbele zaidi. Kwa sababu hii, riwaya ya *Bw. Myombekere na Bi. Bugonoka* inasawiri mamlaka za Mungu Mkuu na miungu wengine wa Kikerewe wanaotambuliwa kwa majina anuai. Mwandishi anataja majina mbalimbali ya Mungu na miungu ya Wakerewe, kama yanavyooneshwa katika Jedwali Na. 1:

**Jedwali Na. 1: Mitazamo ya Wakerewe kuhusu Mungu na Miungu katika Riwaya ya *Bw. Myombekere na Bi. Bugonoka***

| Na. | Jina la Mungu | Mtazamo wa Waafrika na Ufafanuzi |
|---|---|---|
| i | *Namhanga* (uk. 8) | Mungu Mkuu anayetoa ulinzi kamili |
| ii | *Maulana* (uk. 8, 16 na 67) | Mungu Mkuu ndiye mtoaji wa yote. Huyu huwasaidia wenye shida ya uzazi na kuepusha aina zote za laana. |

| | | |
|---|---|---|
| iii | *Karungu* (uk. 453) | Mungu mzimu wa wawindaji wa bara. Huwasaidia wawindaji kupata kitoweo na kuepusha majanga |
| iv | *Kalyoba* (uk. 453) | Mungu mzimu wa jua husaidia kuepusha majanga |
| v | *Mugasa* (uk. 81, 370, 473) | Mzimu wa bahari; mtawala wa bahari au mungu wa wavuvi. Huwasaidia wavuvi na wasafiri baada ya kutoa sadaka ya damu |

**Chanzo:** Kitereza (1980)

Mifano iliyopo katika Jedwali Na. 1 inasawiri maisha ya Wakerewe wanaotambua kuwapo kwa Mungu na miungu yao. Kwa mifano hiyo, makutano ya dini hizi yanadhihirika kwa Wakerewe wanaoamini na kuheshimu miungu kama *Karungu*, *Kalyoba* na *Mugasa* na wakati huohuo wakimwabudu *Maulana* na *Namhanga* kama Mungu Mkuu. Dini ya jadi katika jamii hii inayozunguka Ziwa Viktoria ina historia sitirifu. Kwa mfano, jamii ya Buganda iliyoongozwa na mfalme Kabaka katika karne ya 16 iliamini katika Mungu Mkuu aitwaye *Katonga,* huku *Mugasa* yaani Mungu wa Ziwa Viktoria akipewa heshima ya pekee. Aidha, jamii hii ilikuwa na miungu wengine kama *kiwanuka* (mungu wa radi), *kibuuka* (mungu wa vita) na *muwanga* (mungu wa vilima, jua, mwezi na nyota). Hivyo, makutano ya kidini yanadhihirika bayana kwa kuwa baadhi ya waumini huabudu katika Mungu Mkuu na wakati mwingine waumini haohao huabudu miungu, kiasi cha kuibua imani mseto.

Kama ilivyo katika dini ya jadi, Mungu katika Ukristo, hujulikana kwa majina mengi. Kwa mfano, Biblia inatumia majina mbalimbali kumrejelea Mungu. Baadhi ya majina hayo ni kama *Jehova-jireh* (Mungu Mtoaji, Mwa[3]. 22:8), *Jehova-Nissi* (Bendera yetu, Kut. 14:13-14) na *Jehova-shalom* (Mungu Amani yetu, Amu. 6:22-24). Majina yake mengine ni *El-Shaddai* (Mungu Mtoshelevu, Mdo. 17:28), *Jehova Saboath* (Bwana wa majeshi, Malaki 3:7), *Jehova Tsidkenu* (Bwana ni haki yetu, Yer. 23:6), *Jehova Mekaddishem* (Bwana atutakasaye, Kut 31:13), *Adonai* (Bwana Mwenye enzi yote, Mwa. 15:2-8) na majina mengine mengi. Katika jitihada za kujiimarisha, Wakristo hutumia majina mengine kumrejelea Mungu. Uchunguzi wetu ulibaini kuwa Wakristo wanamtaja Mungu kwa majina kama 'Mwenye nguvu', 'Muweza wa Yote', 'Mfalme wa Milele', 'Yahwe', 'Asiyebadilika', 'Alfa na Omega', na kadhalika. Kwa usambamba huo, mwandishi wa riwaya ya *Mirathi ya Hatari* anabainisha majina anuwai yanayomrejelea Mungu kama yanavyooneshwa katika Jedwali Na. 2.

[3] Majina vitabu katika Biblia huandikwa kwa vifupisho. Kwa mfano: Mwa. ni Mwanzo; Mdo ni Matendo n.k.

**Jedwali Na. 2: Mitazamo ya Wabena kuhusu Mungu katika *Mirathi ya Hatari***

| Na. | Kauli kuhusu Matendo ya Mungu | Mtazamo wa Waafrika na Ufafanuzi |
|---|---|---|
| i | ...Kwa heri Malipula. Mola muhisani akusamehe dhambi zako... (uk.78) | Mungu ni mwenye rehema/huruma<br>-Katika dondoo hili, Gusto anaagana na Malipula anayekaribia kufa. |
| ii | ...Gusto, ya Mungu mengi. Hata hivyo ni vizuri zaidi kwako ukianza kuyasahau polepole... (uk.74) | Mungu ni mwenye mamlaka.<br>-Dondoo hili linaonesha Mwalimu Ericson akimsihi Gusto kumwamini Mungu baada ya kifo cha Dina. |
| iii | ...Mola akupe ustawi wa milele...<br>(uk. 72) | -Mungu ni wa milele. Katika dondoo hili, Gusto anaagana na Dina anayekufa. |
| iv | ...Sote hatma yetu ni hiyo hiyo moja (kufa na kurejea kwa Mola). Hatuna pa kwenda... (uk. 78) | -Mungu ni mhifadhi, baada ya kifo roho hurudi kwa Mungu.<br>-Katika dondoo hili, Mzee Mavengi anamuaga Malipula anayeuawa kwa sihiri. |
| v | ...Lakini hilo si juu yangu kulishtakia, Mungu hutoa mashtaka hayo. Mauaji ya Kapedzile si lazima tungoje Mungu... (uk. 45) | Mungu ni hakimu, jaji, mfalme, Bwana na Mwenyezi.<br>-Katika dondoo hili, Malipula anamuonya Gusto juu ya kifo cha Kapedzile. |

**Chanzo:** Mung'ong'o (1977)

Mifano katika Jedwali Na. 2 inaonesha namna Ukristo na dini ya jadi vinavyopewa nafasi kubwa katika riwaya ya *Mirathi ya Hatari*. Hii inadhihirishwa na majina ya wahusika kama Gusto, Dina na Ericson yakisawiri mtazamo wa Ukristo wakati majina kama Kapedzile (Anayependekezwa), Mavengi (Miti ya Matunda) na Malipula (Mtu mwenye hasira) yanavyosawiri ujadi. Hii ni sawa na kusema kwamba jamii hii ina waumini wanaoabudu katika Ukristo na dini ya jadi kwa nyakati linganifu. Aidha, mwandishi anazidi kushadidia bayana kuwa hata Gusto ni kielelezo cha waumini waliokuwa wakisali kanisani kila Jumapili huku wakiwa ni waumini wa dini ya jadi, katika pango la madhehebu (uk. 34).

Halikadhalika, katika riwaya ya *Kurwa na Doto*, Mungu amepewa nafasi stahiki kwa misingi ya Uislamu. Mtazamo huu unabainishwa na mwandishi kuanzia utangulizi, usawiri wa wahusika na hata maudhui ya riwaya teule. Matumizi ya majina ya Mungu kupitia Uislamu yanasawiriwa katika Jedwali Na. 3:

**Jedwali Na. 3: Mitazamo ya Wamakunduchi kuhusu Mungu katika Riwaya ya *Kurwa na Doto***

| Na. | Kauli kuhusu Matendo ya Mungu | Mitazamo ya Waafrika na Ufafanuzi |
|---|---|---|
| i | Inshallah Mwenye Enzi Mungu atakuvua hili na jingine tena; utazaa kilicho hai, mwana tulee, mji tuzike... (uk. 1) | -Mungu ni mwenye rehema/huruma.<br>-Katika dondoo hili, majirani na masahibu wakimfaraji mama Kurwa kabla ya kujifungua |
| ii | ...Landikwalo ndilo liwalo mja hana hiari... walisahau kuwa mja wa Mungu; na alifahamu kuwa hayo yote yaliyotokea yameandikwa katika *Al-Azal* tangu siku ya kuzaliwa (uk. 29) | -Mungu ni mwenye kujua na kupanga yote<br>-Haya ni maneno ya kumliwaza Kurwa, baada ya Faki kumuoa Doto badala ya Kurwa |
| iii | ...watu walijitahidi kumpa moyo asahau, akumbuke kuwa hayo ni makadara ya Mwenye Enzi Mungu na binadamu hawezi kuyazuia... (uk. 41) | -Mungu ni mkuu na mwenye mamlaka.<br>-Katika dondoo hili mwandishi anafafanua mateso ya Kurwa baada ya mchumba wake Vumbwe kupotelea majini. |

**Chanzo:** Farsy (1960)

Pamoja na data hii ya Jedwali Na. 3, uchunguzi wetu umebaini kuwa Kurani inatambua kuwapo kwa majina takribani 99 yanayomtaja Mungu, yakiwamo *Allah* (Mwenyezi Mungu, Mungu Mmoja), *Ar-Rahiimu* (Mwenye kurehemu), *Al-Qudduusu* (Mtakatifu), *Al-Muhayminu* (Mwangalizi wa viumbe wote) na *Ar-Rauufu* (Mpole na Mwenye huruma), kwa kuyataja machache. Hata hivyo, majina yanayosikika na kutumiwa zaidi na waumini wa dini hii ni pamoja na *Allah*, *Mola*, *Jalal*, *Rabbi*, *Rabbana* na *Rabuka*. Kwa ujumla, mitazamo ya waandishi wa riwaya teule na hata waumini wa dini inaonesha kuwa dini zote zinamtambua Mungu kwa majina mbalimbali.

Makutano ya dini ya jadi na dini za kigeni yanadhihirika katika miktadha tofauti. Kwa kuwa dini zote zipo katika mwendo wa kimageuzi, waumini wa dini ya jadi hushawishiwa kubadili ama kuacha imani zao na kujiunga na dini za kigeni. Vilevile, dhana za kijadi kama kuombea wafu na hata kusafisha makaburi yao, zinaweza kuchukuliwa na kutumiwa na baadhi ya dini za kigeni. Wakati mwingine, dhana fulani za kijadi hupewa tafsiri na dhima mpya ili zikukubalike katika teolojia ya dini za kigeni.

## 3.2 Matumizi ya Mandhari, Maleba na Vifaa vingine vya Kidini

Mandhari, maleba na vifaa mbalimbali hutumika kukamilisha ibada za kidini. Tangu jadi, dini ya Kiafrika hutumia mandhari asilia kama mahekalu, madhabahu,

milima, misitu, mito kama mahala pa kuabudu. Katika mandhari hizi asilia ibada huongozwa na wafalme, machifu na wazee wa mila ama kaya bila kujali jinsia. Katika mandhari hizo, waumini huwasilisha maombi, tambiko, hutoa karipio, kafara ama kufanya manuizi kadiri ya mahitaji. Riwaya teule zinasawiri matukio haya ya kijadi. Kwa mfano, riwaya ya *Mirathi ya Hatari* ni masimulizi kuhusu suala la utoaji kafara katika mapango yaliyofichwa ndani ya vilima vya Njombe. Mwandishi anasema:

> ...ndani ya vilima hivyo hadi leo kuna mapango madogo madogo mithili ya nyumba. Kwa ndani kabisa kuna ukumbi mpana... Humo yasemekana waliponea Wabena wengi nyakati za utumwa na vita vya Wangoni na Wadachi. Zama za mababu habari za mapango haya zilibaki ni siri ya wazee wa kabila... (uk. 15)

Dondoo hili linashabihiana na maelezo ya watoataarifa kutoka Njombe kuwa huko Njombe kuna msitu maalumu wa *Nyumbanitu*, mahali panapofanyika masuala anuwai ya kijadi. Jina *Nyumbanitu* linamaanisha “nyumba nyeusi.” Madhababu haya yapo katika kijiji cha Mlevela, kata ya Mdandu, tarafa ya Igwachanya, wilaya ya Wanging’ombe. Amali ya *Nyumbanitu* ni kuwapo kwa tambiko linalohusisha utoaji sadaka ya wanyama wenye rangi nyeusi kama ng’ombe, kondoo au kuku. Kifalsafa, rangi nyeusi ni ishara ya kuwapo kwa mizimu ya ukoo sawa na utambulisho wa utamaduni wa Wabena. Vilevile, *Nyumbanitu* ni madhabahu yenye kutawala imani, mila, historia na urithi wa maarifa ya jadi. Aidha, *Nyumbanitu* ni nyumba ya uganga kwa kuwa msitu huu hutumika kuchimba dawa za mizizi, magome na majani. Sanjari na msitu wa *Nyumbanitu*, katika eneo hili la Mlevela kuna madhabahu ambatani yaitwayo mapango ya *Manga*. Mapango haya yanapatikana takribani kilometa moja kutoka msitu wa *Nyumbanitu*. Kuwapo kwa maelfu ya popo katika mapango haya kunafanya kijiji cha Mlevela kuwa ni mandhari ya pekee.

Kiulinganifu, Ukristo nao hutumia makanisa, mahekalu na masinagogi yenye madhahabu na altare faafu. Mandhari hizi na mamlaka zake huongozwa na maaskofu, mapadre, mitume, manabii ama wachungaji. Kundi hili husimamia sheria na mamlaka zilizoasisiwa na mitume wa mwanzo kama Yesu Kristo. Aidha, mandhari hizi hupambwa kwa mitindo na rangi zinazobeba dhima mahususi. Kwa mfano, katika Kanisa Katoliki, rangi ya vazi la kasisi ‘kasula’ wakati wa ibada na mapambo yake hutegemea Kalenda ya Kiyahudi na kipindi cha mwaka kilitrujia. Rangi nyeupe huvaliwa wakati wa maadhimisho ya kuzaliwa kwa Kristo na kipindi cha Pasaka. Pia, huvaliwa wakati wa kuadhimisha sikukuu za watakatifu ambao hawakuuawa. Kwa upande mwingine, mavazi ya rangi nyekundu huvaliwa kuashiria damu iliyomwagika wakati wa mitume na mashahidi wengine wakitetea imani. Vilevile, rangi ya zambarau huvaliwa kipindi cha mfungo wa siku 40 maalumu kama “Kwaresma”. Aidha, rangi ya kijani na rangi ya dhahabu hubeba dhima mahususi katika kanisa.

Kwa usambamba, dini ya jadi na hata ya kigeni, hutumia zaidi maleba ya rangi nyeupe, nyekundu na nyeusi. Rangi hizi hubeba maudhui ya kiontolojia kulingana na dini husika. Kwa mfano, katika riwaya ya *Kurwa na Doto*, tunaelezwa kuwa rangi tatu zilitumika kumpamba ng'ombe wa kafara katika tambiko la kukoga mwaka, kama asemavyo mwandishi:

> ...Kadhalika, siku hiyo makohani baada ya kutazamia waliona ya kuwa mji utataka kuzinguliwa kwa dhakiri na Kurani pamoja na kuzungushiwa ng'ombe mwenye rangi tatu, weupe, weusi na wekundu... (uk. 25).

Dondoo linasawiri fikra za Swantz (2014) asemaye kwamba kwa kawaida mandhari za kijadi hunuizwa kwa rangi nyeupe, nyeusi na nyekundu. Kama tulivyosema awali, uteuzi wa rangi ya vazi au madhabahu hutawaliwa na dhima, itikadi na falsafa mahsusi.

Katika mandhari za kijadi kuna matumizi ya vifaa na viumbe wenye kuongeza nguvu-hai ya ulimwengu. Vifaa hivi ni kama hirizi, damu, vyungu, vyetezo, ngoma, mgwisho, chepeo, kucha, ubani na mikoba ya uganga. Viumbe teule kama majini na mizimu huweza kutumika ili kuongeza nguvu-hai kiutendaji. Pia, katika dini za kigeni kuna matumizi ya vyetezo vya ubani, mishipi, slota, rozari na mapiku. Nyenzo nyingine zinazotumiwa kama kinga ni maji ya baraka, mafuta matakatifu, majivu na mishumaa. Nyenzo hizi hutumika kuongeza nguvu-hai ya Ukristo na dini za nyingine za kigeni ni mwigo wa nyenzo za kijadi. Hii ni kwa sababu tangu jadi vyetezo na ubani vilitumiwa katika matukio ya kidini na kiganga wakati wa kuzindika mji ili kufukuza majini na mapepo.

Masuala ya kimiujiza yaliyofanyika katika dini ya jadi pia yanafanyika katika dini za kigeni. Kwa mfano, vifaa vya kidini na kiuganga vya kila aina huuzwa kila mahali siku hizi. Watu bado wanaonekana wakivaa, wakining'iniza katika mazizi ya mifugo au kufukia nyumbani mwao. Vifaa vyenye maumbo kama hayo vinauzwa hivi leo kanisani na misikitini. Aidha, hirizi kama zilivyo rozali au tasibihi hushabihiana kimatumizi. Hirizi ni kifaa kinachomkinga mwanadamu dhidi ya shambulio la ugonjwa au hatari. Kwa mujibu wa Mutiso (2012) hirizi huwa na nguvu za miujiza na uchawi na humkinga mtu dhidi ya hatari na mikosi kama kifo, mapepo wabaya, ulozi, macho ya husuda, radi, kuvunjika kwa chombo cha ubaharia, shambulio la wezi, wanyama hatari, na kadhalika. Hirizi kama zilivyo rozari huning'inizwa shingoni, mabegani, mikononi, kwapani, miguuni na viunoni kama kinga ya hatari. Kama inavyoelezwa katika Biblia, Kurani ama katika miiko ya kijadi, vifaa hivi hutumika kama kinga kwa waumini ili wasiangamizwe na waovu. Tunaweza kuhitimisha hoja hii kwa kusema matumizi ya mandhari, maleba na vifaa mbalimbali hutumiwa na dini zote kukamilisha ibada ambazo huenda sanjari na uimbaji, uchezaji na upigaji ngoma.

### 3.3 Dhima za Dini kwa Ujumla

Kama ilivyosemwa awali, dini ya jadi na za kigeni zina maudhui ya jumla ambayo hayapingani kwa kiasi kikubwa. Dini hizi zinapatana ijapokuwa mapatano hayo si rasmi. Kwa mtazamo wetu, dini ya jadi ilikwishajenga misingi kabla ya maijilio ya dini za kigeni. Tangu jadi, dini ya jadi iliumba fikra, mithiolojia na imani ya kumtambua Mungu. Pia, suala la maadili husisitizwa katika dini ya jadi kama ilivyo katika dini za kigeni. Aidha, dini zote zinapiga vita uzinzi, wizi, mauaji, chuki na uongo. Kwa ujumla, dini zote zinahubiri utu unaojumuisha upendo, uvumilivu, ukweli, unyenyekevu, uaminifu, ushirikiano, utii, matendo ya huruma na kuheshimu wakubwa.

Katika kuzidi kujiimarisha, dini zote huwa na siku maalumu kama kuadhimisha kuanza mwaka, kuwakumbuka wahenga wao ama kumbukizi nyingine za kiimani. Kwa mfano, katika riwaya ya *Kurwa na Doto*, siku ya Mwaka-kogwa hutumiwa na Wanamakunduchi kuwakumbuka na kuwaenzi wahenga na mizimu yao kwa maombi na sadaka. Katika riwaya hii, mwandishi anasema:

> ...Sherehe ya kukoga mwaka ilipowadia, Vumbwe alimtaka Kurwa na mama yake wafuatane naye wende shamba lililo karibu na pwani wakaukogee shambani huko. Kurwa na mama yake waliona uzito kwenda na walimnasihi Vumbwe avunje safari ya shamba wakoge mwaka pale pale mjini, lakini Vumbwe alikataa na kushikilia wende. Alisema huko wataona mambo mengi ambayo mjini hayafanywi, kama vile kuchoma kibanda na mtu ndani yake katika saa sita za mchana wa kukoga mwaka, vigongo yaani upiganaji wa vigongo baada ya kuchoma kibanda, na mengi mengineyo... (uk. 22).

Mambo yanayosisitizwa katika siku hiyo ni kuuzindika mji usishambuliwe na majini, kuzuru mizimu, kuchapa machenga, utambaji nyimbo na kuchoma kibanda cha Mwaka. Matukio haya yana dhima mahususi kifalsafa (taz. Mpalanzi, 2019; Khamis, 2019). Katika dini ya Ukristo kuna sherehe za kumbukizi kama *Krismasi* na *Pasaka* ilhali katika Uislamu kuna sherehe kama *Id el Haji* na *Id el Fitri*.

Kama ilivyoelezwa awali, dini hizi zinatumika kwa usambamba huku dini ya jadi ikiota mizizi vijijini wanakoishi Waafrika walio wengi, na dini za kigeni zikitamalaki mijini. Kwa kuwa familia na jamii ni kiini cha dini zote, kila dini hupambana kutoa miongozo na itikadi zinazoshughulikia maisha na mwono-ulimwengu kwa ujumla.

### 3.4 Suala la Utendaji na Utoaji Sadaka

Kwa kuzingatia ontolojia ya Kiafrika, sadaka hutolewa kwa miungu, mizimu na wahenga. Kundi hili hutambuliwa kama wakuu wa familia na koo, kwa kuwa linatokana na wanadamu walioishi duniani. Kwa sababu hii, Mbiti (2011a) huwaita "wafu-wanaoishi" kuwa ni kundi linaloishi na watu hai huku likiwa na jukumu la kuwapatanisha na Mungu. Bado ni vigumu kuelezea tajiriba faafu za wahenga na

mizimu. Itoshe kusema kuwa wao ni wapatanishi kati ya Mungu na wanadamu. Jukumu la wapatanishi hawa ni kupokea maombi na sadaka kadiri zinavyowasilishwa na wanadamu. Katika kufafanua suala hili, mwandishi wa riwaya ya *Kurwa na Doto* anaona kuwa utoaji sadaka ni ada za msingi ambayo huwakutanisha wanadamu, miungu na wahenga. Kwa mfano, Wamakunduchi huwakumbuka wahenga na mizimu kwa kuwatolea maombi na sadaka, kama mwandishi anavyofafanua:

> ...Siku moja kabla ya kukoga mwaka, mizimu, mapango na makaburi yalisemezwa na kupewa ada zao. Vijuzuu vyao walisoma khitma kwanza, kukhitimishwa na wazee. Baadaye alitolewa ng'ombe mwenye sifa zilizotakiwa kafunikwa shuka, kaniki na bendera na kuning'inizwa hirizi usoni. Hirizi hiyo ilikuwa imening'inizwa kwenye pembe. Kutoka hapo, jaha na mkururo wa watu uliondoka, ng'ombe mbele vyetezo vya ubani na uvumba, pamoja na marashi na majimbo vimechukuliwa ubani kulia na kushoto mwa ng'ombe. Mkururo ulizuru mapango, mizimu na makaburi yote. Mwishowe, waliishia pwani ambako ng'ombe alichinjwa na damu kuachiwa kutelemkia majini. Kichwa cha huyo ng'ombe kilichukuliwa kwa shangwe kikapelekwa kwenye pango kuu (kur. 25-26).

Katika dondoo hili, mwandishi anasisitiza kuwa utendaji wa tambiko huenda sambamba na uchinjaji ng'ombe wa kafara. Ng'ombe huyu hutolewa kafara kama sadaka kwa 'Bwana Mwaka' ili asiangamize watu. Hii ni sawa na kusema wanyama hutolewa sadaka kwa miungu, mizimu au wahenga kama ishara ya kuwakumbuka ili miungu wabaya wasiwaangamize wanadamu. Katika riwaya ya *Mirathi ya Hatari*, utendaji wa tambiko unakwenda sambamba na masuala ya sihiri na imani za kichawi. Hivyo, Gusto analazimika kufanya tambiko la kafara linalomuingiza katika jumuiya ya wachawi ili aweze kurithi sihiri na madawa ya baba yake. Mwandishi anasema:

> ...tulimaliza kulivinjari pango lile. Tukawa tunarudi kwenye pango la madhehebu... Mvyele akasimama akasema, 'Kama mjuavyo madhehebu hasa hayajaanza. Mambo yenyewe yatafanyika hasa Jumamosi ya juma la pili tangu leo. Na kufuatana na jadi yetu mgeni wetu itampasa ajiandae kutoa *kipongo*. Na ili dawa ziweze kufaulu *kipongo* huyo sharti awe wa damu... (uk. 27).

Katika dondoo hili, mwandishi anadhihirisha kuwa tambiko la *kipongo*[4] ni tukio la umwagaji damu. Gusto anaamua kutoa *kipongo* kwa kumuua mjomba wake Kapedzile Mwanangoha kama kafara ili aweze kurithi milki na utawala wa baba yake.

Katika riwaya ya *Bw. Myombekere na Bi. Bugonoka*, Myombekere na mkewe Bugonoka wanaomba dua kwa mizimu huku Myombekere akishika mkuki uitwao *nabuhotora* upande wa kushoto na kushika beberu upande wa kulia.

[4] Hili ni tambiko la kafara la kupokea uchawi.

Tambiko hili lilinuia kutoa sadaka ili kumjalia afya njema mtoto wao, Ntulanalwo. Katika, tambiko hili Myombekere ananuiza maneno kumtambikia Ntulanalwo aliyekuwa mapajani mwa Bugonoka akisema:

> ...pokea mbuzi wako, ni huyu, tunayekupa kukuchinjia, upate ngozi yako ya kukubeba, ikupe afya... Enyi fulani na fulani, nanyi wazee wetu nyote wa ukoo wetu nyote kwa jumla, kutanikeni nyote mhudhurie hapa, mpokee mbuzi wa mtoto, tunayetaka kumchinja ngozi ya kumbebea, apate heri na afya njema maishani mwake!... (kur. 334-335). Nyinyi wazee wetu nyote mliokufa, karibuni, mpokee kitoweo chenu vizuri mlichotayarishiwa hapa, na mtoto wenu huyu Ntulanalwo, tunaomba msimletee madhara katika ngozi yake hii ya kutembea, tuliyomchunia leo hii, adumu kuishi daima mwenye afya njema, atembee maishani mwake katika ardhi, mchwa anajitenga!... (uk. 337).

Katika dondoo hili, mwandishi anafafanua namna tambiko la kumtoa mtoto linavyokwenda sambamba na utoaji sadaka kwa miungu. Watambikaji hunuia kumwepusha mtoto dhidi ya maovu. Aidha, tambiko hili hutumika kama sadaka na kinga ya watoto dhidi ya miungu wabaya.

Katika dini ya jadi, watendaji wakuu huwa wanaweza kuwa wanaume au wanawake kutegemea mfumo wa kijamii. Lakini, katika baadhi ya makanisa hasa Katoliki na hata misikitini watendaji wakuu madhabahuni huwa ni wanaume. Viongozi hawa huongoza ibada zenye ushawishi, huamsha hisia, jazba na mihemuko mbalimbali, na kupokea sadaka. Tukio la utoaji sadaka katika dini za kigeni linaonekana kuwa ni mwigo wa dini ya kijadi. Katika Ukristo kwa mfano, msingi wa utoaji sadaka katika dini hizi ni kisa cha Ibrahimu na mwanae Isaka. Kwa mfano, katika Biblia, Mwanzo 22:2-13 kuna masimulizi kuhusu kisa cha Ibrahimu kumtoa sadaka mwanae wa pekee Isaka awe sadaka ya kuteketezwa. Baada ya kupimwa imani ile, Mungu akamzawadia kondoo akisema “tazama kondoo mume yuko nyuma yako amenaswa pembe katika kichaka”. Sanjari na hili, katika Mithali 3:9-10, Biblia inahimiza mwanadamu kufanya agano na kutoa sadaka ya malimbuko ya mazao ili aweze kupata mazao mengi ghalani. Kwa sababu hii, Mpalanzi (2019) anadai kuwa majilio ya dini za kigeni, sanjari na utoaji sadaka yanaonekana kuongezewa ‘nguvu za kichawi’ na kubuniwa mikakati mingi ya utoaji sadaka hasa mijini kwenye waumini wengi. Aidha, wahanga wa uchawi, magonjwa, ugumba, vifo, mikosi, kiwewe na majanga hulazimika kutoa sadaka kamili ili kutia msukumo katika maombi na uponyaji. Hapa tunaona kuwa suala la utoaji sadaka limepewa kipaumbele katika dini za kigeni kama ilivyo katika dini ya jadi.

### 3.5 Miiko ya Kijadi kama zilivyo Amri za Mungu

Miiko ni miongozo ya makatazo ambayo watu au jamii hawaruhusiwi kutenda kulingana na imani, tajiriba au kaida fulani. Kwa kawaida, miiko hutumiwa ili kutambulisha itikadi au falsafa inayotawala jamii husika. Makala hii inabainisha

kuwa kila jamii ina miiko ambayo inasimama kama sehemu ya utambulisho, falsafa na itikadi. Kwa mfano, katika riwaya ya *Bw. Myombekere na Bi. Bugonoka*, mwandishi anaonesha namna Wakerewe wanavyoheshimu baadhi ya viumbe wasio wanadamu. Mwandishi anaeleza kuwapo kwa mzimu mwenye umbile la nyoka mwekundu anayedondoka darini wakati Myombekere na mkewe wakiwa katika tambiko la *ebisisi*, katika jumba la matambiko. Yowe la mkewe, linamfanya Myombekere aruke moto wa *ekikome* ili kuwaokoa watu wasing'atwe na nyoka. Hata hivyo, Myombekere anapotaka kumuua nyoka huyo anakatazwa na mkewe, Nkwazi kuwa nyoka wa ndani huwa si kiumbe wa kawaida, bali ni mzimu anayekuja kutaka kusemeshwa. Kama Bugonoka anavyomwambia Myombekere:

> ...Ehe, umekuwa mwehu leo? Uue nyoka kweli! Na wewe mtu mzima hivi...Au kwa kuwa huzai, ndiyo sababu unataka kuua nyoka?...Wewe huogopi balaa kwa siku za usoni?... Hayo ni ya kweli azoeaye kuua nyoka hakosi kupatwa na balaa, hapana. Kumbe wewe usilogwe ukathubutu kuua chatu… hata mimi nayasema tu kwa mzaha... siwezi kamwe kuvunja kanuni ya watu wote... (kur. 144-145).

Hapa Myombekere anajisahaulisha tamaduni za Kikerewe huku akitambua kuwa tangu jadi, chatu ni sehemu ya imani ya utamaduni wao. Hata hivyo, inaaminika kuwa chatu ni sehemu ya miungu ya jadi ya Wakerewe. Kwa Wakerewe, chatu anayeonekana ndani ya nyumba huwa hauawi kwani Mkerewe akimuua chatu anapaswa kuwa na mtoto atakayempa jina la chatu, vinginevyo mtoto wake mmojawapo atafariki.

Pia, ilielezwa kuwa nyoka aina ya "swila wa majini" akikuuma ndani ya maji ni mwiko kutoka nje ya maji sharti ubaki humohumo majini mpaka mganga afike. Vinginevyo, utokapo utapata uchungu mwili mzima na kufa hapohapo (kur. 450-451). Vilevile, ipo miiko inayokataza kula baadhi ya vyakula ama vinywaji katika jamii ya Wakerewe. Katika mazingira mengine wanaweza kula kwa kufuata masharti fulani. Kwa mfano, wanawake ni mwiko kula samaki waitwao *ensonzi, embozu, kambare-mamba* na *embete* (kur. 412-413). Samaki wa aina hii huwa ni maalumu kwa wanaume tu.

Kadhalika, ipo miiko ya Wakerewe inayohusu taratibu za vyakula. Katika mila na desturi za Wakerewe, wanawake na wanaume hawaruhusiwi kula pamoja. Pia, kijana aliyeoa katika ukoo fulani haruhusiwi kula meza moja na baba mkwe. Katika suala hili, Myombekere anafafanua namna alivyokwenda kuomba radhi ukweni, na huko walipoivisha chakula walimtengea chakula chake, naye baba mwenye mji akatengewa peke yake. Mwandishi anasema:

> …Bugonoka, akatia unga ndani na kusonga ugali ulipokuwa tayari akauipua na kuugawa sehemu mbalimbali: ule wa wanawake akautia katika kikapu kidogo, wa baba mji nao akauweka mbali, sababu hiyo si desturi ya Abakerebe mtu kula pamoja na mkwe wake, na ule wa mume wake na shemejiye Lweganwa, akautengeneza sawa sawa...(uk. 55).

Dhima ya miiko ya ukaaji wakati wa chakula katika jamii ya Wakerewe ni kudumisha utu, heshima na kuhifadhi tamaduni za jamii. Kwa misingi ya Kiafrika, baba mkwe na mama mkwe hupewa heshima stahiki. Pia, mwandishi anaeleza miiko inayozuia watu wenye koo za utani kutaka kuoana. Mwandishi anasema wakati Myombekere anarudi nyumbani kwake kutoka ukweni kuomba radhi, alikutana na mwanamke aliyekwishaachika kwa mume wake kwa kosa la kutozaa (*musimbe*). Baada ya mazungumzo ya kutambulishana koo, Myombekere anaanza jitihada za awali za kutaka uchumba na kumposa, na ndipo anabaini kuwa ipo miiko iliyowazuia wawili hao kuoana. Yule bibi akanena:

> ...imekuwa haramu kabisa kwa sababu ukoo wa mume wake huo ndiyo watani wetu hasa…ule ugonjwa wa *olugurwe* hapana hasha! Ujitupe motoni nawe unajua utaungua! Hiyo haifai kabisa...Walipokwisha kuona kipingamizi cha kuoana, yaani mwiko mkubwa sana kwa Abakerebe, walipeana kwa heri... (uk. 22).

Katika dondoo hili, mwandishi anatanabahisha kuwa Wakerewe wanaamini kuwa ukioa au ukiolewa na mtani wako utaugua ugonjwa uitwao *olugurwe* (ugonjwa wa utani). Ugonjwa huu ni hatari sana kwani hauna tiba. Mwandishi anaona kuwa ni afadhali kupata ugonjwa wa *olwihwa* (ugonjwa wa kumuoa mpwa) kwa kuwa huo unaponywa kwa mitishamba. Hivyo, mwandishi anawashauri vijana wazitambulishe koo zao kabla ya kuoana. Kadhalika, ipo miiko inayowataka watu kuzingatia taratibu za kuzikana na kuheshimu maziko.

Katika riwaya ya *Kurwa na Doto*, mwandishi anadai kuwa jamii ya Makunduchi ina mwiko kwa mwanamke mwenye mimba kupishana na mtu aliyechukua moto, kwa hofu kuwa mwanamke huyo anaweza kukatishwa uzazi wake (uk. 1). Vilevile, imeelezwa kuwa ipo miiko inamkataza mwanamke wa Kiislamu kufika makaburini kuzika (uk. 38). Aidha, ipo miiko mingine inayofungamana na jadi ya makuzi ya mtoto baada ya kuzaliwa, ikiwamo kufanyiwa zeyazeya, kuvunjiwa nazi na kunyunyiziwa maji, kutembezwa kila pembe ya nyumba hadi kizingitini na kushindiliwa roho. Miiko na ada nyingine ni pamoja na kutiwa nyungoni na kukalishwa juu ya ungo wa mchele (uk. 3-4). Dhima ya miiko hii ni kutunza maadili na utamaduni wa jamii.

Ama kwa hakika, miiko ni kipengele cha kimaadili katika ontolojia ya Kiafrika. Jamii isipozingatia miiko hiyo, hukumbana na nguvu za kiulimwengu. Pamoja na kutambua umuhimu wa itikadi zilizofumbatwa katika miiko, bado kipengele hiki hutumiwa na waandishi wa fasihi kukamilisha maudhui katika riwaya teule. Hata hivyo, baadhi ya miiko hii imeanza kufifia kutokana na mwingiliano wa dini za kigeni, ukuaji wa miji na athari ya elimu ya Kimagharibi.

Kwa upande mwingine, dini za kigeni zimesheheni miiko, amri, sheria na makatazo mengi. Maandiko yanaeleza kuwa Mungu alipomuumba mtu, alimwekea miiko hiyo ili aweze kutenda mema. Kwa mfano, katika Kut. 20:1, Biblia inafafanua bayana amri za Mungu. Katika Biblia kama ilivyo Kurani, kuna

maagizo ya Mungu ya kuwataka wanadamu wazingatie maadili na watimize wajibu wake.

### 3.6 Dini na Suala la Maisha

Dini zote humwekea mwanadamu misingi muhimu ya maisha. Kwa mfano, riwaya ya *Kurwa na Doto* inathibitisha kuwa baadhi ya waumini hutumia mizimu na imani za kijadi kama msingi wa maisha (uk. 5 na 22). Vilevile, utoaji kafara kwa miungu kama alivyofanya Gusto katika riwaya ya *Mirathi ya Hatari* ilimsaidia kujijengea ustawi katika ulimwengu wa sihiri katika pango la madhehebu (uk. 27 na 44). Aidha, mwandishi wa *Bw. Myombekere na Bi. Bugonoka* anaonesha kuwa maombi kwa mizimu husaidia kuleta ustawi wa uzazi na familia pana. Dini ya jadi, hasa tambiko hutumika katika mazishi, na huwalinda ndugu wa marehemu kwa kuwa mfu asipozikwa vizuri safari yake huishia njiani, na roho ya mfu huwaathiri walio hai (uk. 331, 540 na 565).

Naye Mbiti (2011) anasema popote alipo Mwafrika pana dini yake. Kwamba, dini ni asasi muhimu inayotawala mfumo wa maisha ya mtu katika idara zake. Mbiti (khj) anakiri kwamba dini ni asasi yenye nguvu kuliko asasi nyingine za kiitikadi kwa kuwa huathiri fikra za watu. Kwa maoni yake, Mwafrika popote alipo hutumia dini kama vile katika kilimo, matanga, chuoni na hata bungeni. Anafafanua:

> ...Kwa sababu dini za jadi zinajipenyeza kila nyanja ya maisha, hakuna tofauti ya maisha ya utakatifu na ya kidunia, kati ya maisha ya kidini na yasiyo ya kidini, na kati ya maisha ya kiroho na ya kimwili. Kila alipo Mwafrika kuna dini yake: anakwenda nayo shambani anaposia mbegu au kuvuna mazao mapya; anakwenda nayo kwenye pombe au anaposhiriki katika mazishi, na kama ameelimika, atakwenda nayo katika chumba cha mtihani shuleni au chuo kikuu; kama ni mwanasiasa atakwenda nayo bungeni... (Tafsiri yetu)

Dondoo hili linaonesha kuwa dini zote hutumika wakati wa raha na tabu. Kwa mfano, dini ya jadi imekuwa urithi tangu kale kwa kuwa imeshikamanisha watu, matukio, nyakati na maisha ya umilele. Dini hii si ‘masalia’ ya matukio yaliyopita bali imefungamana na imani halisi na utambulisho wa Mwafrika. Kadhalika, Ukristo na hata Uislamu umefungamana na maisha ya mtu tangu kuzaliwa, kuishi na kifo.


Kadhalika, waumini wa dini zote wanaamini kuwa maisha ya mwanadamu hapa duniani hayana umilele. Dini zote zinaamini kuwa kifo hakiepukiki hata kama mtu ataishi maisha marefu kiasi gani. Kwa misingi ya dini ya jadi, maisha ni mapito kutoka ulimwengu wa kawaida kuelekea ulimwengu wa mizimu. Misingi ya Ontolojia ya Kiafrika inazingatia imani kuwa baada ya kifo roho za wafu huendelea kuwapo ulimwenguni. Kwa mujibu wa Ontolojia hiyo, nafsi ya mtu imejengwa na elementi mbili za msingi yaani mwili na roho. Wakati wa kuzaliwa mtu, mwili na roho huungana. Roho hiyo huendelea kuwapo katika mwili wa mtu

katika kuishi kwake. Baada ya mwili kufa, roho kuendelea kuwapo ulimwenguni na kuungana na miili mingine. Akifafanua dhana hii, Mihanjo (2004) anasema:

> ...Roho ya binadamu hutoka katika ulimwengu wa roho. Roho hiyo hushiriki katika akili na mawazo ya jumla na huunganishwa na mwili, lakini huwa si kitu kimoja na mwili. Hata hivyo, baada ya kifo, roho haifi. Kwa sababu hiyo, roho hutoka katika mwili mmoja na kuingia mwili mwingine. Hii ni kwa sababu roho ni kitu ambacho hakina umbisho. Hivyo, roho ni kitu ambacho hakiwezi kuharibiwa...

Maelezo haya yanafafanua kuwa Wabantu huzingatia kanuni ya kimetafizikia ya uhamisho wa roho. Kanuni hii inaelekeza namna roho inavyohama katika mwili unaokufa na kuzaliwa upya katika mwili mwingine. Mchakato huu hufanyika kwa kuwa roho haiwezi kukaa mahali pasipo mwili. Kwa kuwa mfu ni sehemu ya ukoo na jamii, roho ya mfu inaweza kuhamia, kuzaliwa, kutunzwa na kutenda kazi ndani ya ukoo na jamii. Hii ni sawa na kusema roho hiyo huwa katika mwendo na umbo la kiduara kupitia hatua nne za kiontolojia kama zinavyoonekana katika kielelezo Na. 1:

**Kielelezo Na. 1: Ontolojia ya Kiafrika kuhusu Roho ya Mtu katika Mwendo**




**Ufunguo**
Hatua A: Kuungana kwa Roho na mwili
Hatua B: Utendaji kazi wa roho katika mwili
Hatua C: Utengano wa roho na mwili baada ya kifo
Hatua D: Roho kuungana na mwili mwingine na mfu kuungana na wahenga

**Chanzo:** Mpalanzi (2019: 240)

Kama ilivyoelezwa awali, kifo si mwisho wa maisha ya mtu duniani. Wabantu wanaamini kuwa baada ya kifo, kuna mchakato wa namna jamii inavyomkabidhi mfu kwa wahenga. Ilielezwa kuwa katika jamii ya Wabena, mchakato huu

huchukua kipindi cha miongo kadhaa. Kwa mfano, Wabena huamini kwamba wafu huwa na safari ndefu katika kuifikia ardhi ya wahenga. Mchakato huanza kwa mfu kuzikwa na vifaa vya kijadi kama mshale, upinde, rungu, mundu au shoka. Vifaa hivi hutumika kama silaha za ulinzi wake akiwa safarini. Wengine humzika mfu pamoja na vyakula, vinywaji au vifaa vya nyumbani kama majembe, mikeka na vyungu wakiamini kuwa vitatumiwa na mfu akiwa katika ulimwengu mwingine. Jamii hii inashikilia imani kuwa kumzika marehemu bila mali, vifaa au zawadi ni sawa na kumfukia kama mnyama. Mchakato huo hukamilishwa kwa tambiko maalumu la kijadi ambalo hufanyika ili kumkabidhi mfu kwa wahenga. Tambiko hili huambatana na utoaji kafara ya mnyama ambapo damu, mifupa na nyama huashiria chakula na zawadi kwa wahenga.

Baada ya miongo na vizazi kadhaa, mfu hubadilika taratibu kutoka hali ya sasa kwenda zamani. Hii ina maana kuwa baada ya tukio halisi la kufa, mfu huwa katika wakati wa "sasa" na mfu huwa hatoweki ghafla miongoni mwa ndugu zake, kwani huendelea kukumbukwa kwa jina, tabia, matendo, kufanya tambiko na kupokea miongozo. Kinyume chake ni mtu-mfu, yaani yule asiyeweza kudumisha uhusiano wake na wale walio hai atakuwa amekufa kabisa. Kwa mchakato huu, 'mfu' huaminika kutoweka kabisa baada ya kupita vizazi vinne au vitano na hasa baada ya kifo cha mtu wa mwisho aliyemkumbuka.

Kwa mtazamo tofauti, Kahigi na Mulokozi (1979) katika Mnenuka (2011) wanaamini kuwa maisha ya binadamu yanaanza na yanaishia hapahapa duniani. Kama ilivyo kwa viumbe hai wengine, baada ya kufa binadamu huoza na kuwa udongo, na ndiyo mwisho wa historia ya maisha ya binadamu. Hii ni sawa na kusema maisha ya mwanadamu hupotea kama moto unavyopotea ukizimika. Mulokozi (2017) anaona kuwa pamoja na kuwapo kwa fikra za maisha baada ya kifo, maisha hayo ni dhahania kwa kuwa maisha halisi ni ya hapa duniani. Mtazamo wetu katika makala hii ni kuwa ijapokuwa Wabantu wanatambua suala la kuwapo kwa maisha baada ya kifo,maisha hayo hayathaminiwi kuliko maisha ya sasa. Kwa sababu hii, Mulokozi (khj) anasonga mbele akidai hakuna pepo wala jehanamu na wala hakuna tunzo wala adhabu baada ya kufa. Kwamba, mtu hutunzwa au kuadhibiwa awapo hapa hapa duniani. Mwanadamu akifa ndiyo mwisho wa maisha yaliyo halisi.

Kwa upande mwingine, dini za kigeni, zinaamini kuwapo maisha ya kiroho baada ya kifo. Kwa imani ya dini za kigeni, mtu aliyeishi duniani bila dhambi, atakapokufa ataishi maisha mengine katika ulimwengu wa kiroho. Kurani inaitetea hoja ya kuwapo kwa maisha baada ya kifo. Mtazamo huo unatetewa na kauli ya Allah aliposema: "Kila kilicho juu ya ardhi ni chenye kufa" (taz. Surat Al-Rahman, aya ya 27). Kwa mtazamo huo, Uislamu unaamini maneno ya Allah anavyosema: "Kila nafsi itaonja umauti" (taz. Surat Al-Anbiya, aya ya 35). Kama ilivyo desturi hakuna uhai usiokuwa na mauti. Uislamu unaamini kuwa siku ya kufufuka, mfu atarudishiwa uhai wake na kuhukumiwa kutokana na matendo yake

duniani. Kwamba, watenda mema watakwenda mbinguni, na waovu watakwenda motoni kuadhibiwa.

Kadhalika, Biblia Takatifu inafundisha teolojia na imani ya kuwapo kwa maisha baada ya kifo. Hapa tutatoa mifano michache, katika Luk. 16:19-31, kuna kisa kinachohusu tajiri na maskini Lazaro, watu hawa walipokufa, tajiri alikwenda kuzimu na Lazaro akaenda paradiso. Katika kitabu cha Yohana, Yesu anasema: "Mimi ndiye ufufuko na uzima. Yeye aniaminiye mimi ajapokufa, atakuwa anaishi" (Yoh. 11:23-27). Kundi hili linaamini kuwa mtu akifa hupumzika tu kaburini akisubiri ufufuo wa Yesu, na hapo maisha yake yataendelea tena. Maandiko haya yanasema, "...nao waliokufa watafufuliwa kwanza. Kisha sisi tulio hai, tuliosalia, tutanyakuliwa pamoja nao" (1 Thes. 4:13-18).

Mifano ya hapa juu inaashiria kuwapo kwa makutano ya dini hizi kwani dini zote haziamini maisha ya umilele hapa duniani. Suala la kuwapo kwa maisha baada ya kifo lilikuwapo tangu enzi na lilikuwa msingi wa imani za kijadi. Suala hili limeendelea kupewa msukumo mpya na dini za kigeni, dini iliyoletwa na wakoloni kwa mwamvuli wa umisionari.

## 4.0 Hitimisho

Hoja zilizoainishwa hapa juu, zinaashiria kuwa dini zote ni makutano ya asasi zilizochipuka katika shina moja la ujadi. Hata hivyo, mabadiliko ya dini yanayoonekana katika riwaya teule na hata katika jamii ya leo yanaonesha kuwa dini nazo zimebadilika kutokana na mapinduzi katika uchumi wa fedha, viwanda na sayansi na teknolojia. Masuala haya huwafanya hasa waumini wa dini za kigeni wanaojinasibisha zaidi na uchumi wa mijini kujiona bora kuliko waumini wa dini ya jadi walioshikiliwa na uchumi wa vijijini. Licha ya mgawanyiko huo, bado dini zote zina dhima mahususi na hutumika hasa katika nyakati ngumu za maisha. Hii ni sawa na kusema kwamba Waafrika wengi wanapokumbwa na majanga mazito hukimbilia katika dini ya jadi ama dini za kigeni kwa imani kuwa ni asasi yenye ulinzi kamili. Hata hivyo, licha ya ushikamani huo, dini ya jadi inaonekana kukita mizizi zaidi katika maisha ya Waafrika kwa kuwa dini za kigeni ni mwigo na mwendelezo wa misingi iliyowekwa na dini ya jadi ya Kiafrika.

## Marejeleo


Al-Farsy, S. S. (1991). *Kurani Tukufu* (Tafsiri). Nairobi: Nairobi Islamic Foundation.

Antony, K. 1. (2014). The Meaning and Nature of African Philosophy in a Globalising World, *Journal of Humanities Social Sciences and Education* (IJHSSE), 1: 86-94.

Awolalu. J. O. (1976). What is African Traditional Religion?" *Studies in Comparative Religion*, 10(2): 1-10.

Awolalu J. O. and Dopamu, P. A. (2005). *West African Traditional Religion.* Ibadan: Macmillan.

Chama cha Biblia Tanzania na Kenya (2000). *Biblia: Maandiko Matakatifu*. Nairobi: The Bible Society of Kenya.

Ekeke, E. C. and Ekeopara, E.A (2010). Divinities and Spirits in African Traditional Religious Ontology, *American Journal of Social and Management Science*, 209-218.

Farsy, M. S. (1960). *Kurwa na Doto*: *Maelezo ya Makazi katika Kijiji cha Unguja*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Gyekye, K. (1987). *Tradition and Modernity: Philosophical Reflections on the African Experience*. New York: Oxford University Press.

Kahigi, K.K na Mugyabuso M.M (1979). *Kunga za Ushairi na Diwani Yetu*. Dar es Salaam. Tanzania Publishing House.

Khamis, R. J. (2019). "Dhima ya Mwanamke katika Kuibua Dhamira za Nyimbo za Sherehe za Mwaka Kogwa katika Jamii ya Makunduchi." Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Kitereza, A. (1980). *Bw. Myombekere na Bi. Bugonoka: Ntulanalwo na Bulihwali*. Juzuu 1 & 2. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.

Magesa, L. (1997). *African Religion: The Moral Traditions of Abundant Life*. Nairobi: Pauline Publications Africa.

Mbiti, J. S. (1970). *Concepts of God in Africa*. London: S.P.C.K

_______(2011). *Introduction to African Religion*. Nairobi: East African Educational Publishers Ltd.

________ (2011a). *African Religion and Philosophy*. Nairobi: Heinemann Educational Books Limited.

Mnenuka, A. J. (2011). Falsafa ya Maisha katika Ushairi wa Mugyabuso Mulokozi na Shaaban Robert, *Kioo cha Lugha*. 9:104-121

Mpalanzi, L. (2019). Ujitokezaji wa Falsafa ya Kiafrika katika Riwaya za Kiethnografia za Kiswahili, Tasinifu ya Uzamivu (Haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mung'ong'o, C. (1977). *Mirathi ya Hatari*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.

Mulokozi M. M (2017). *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili: Kozi za Fasihi Vyuoni na Vyuo Vikuu.* Dar es Salaam: Muccony Printing Press.

Swantz, M. (2014). *Uzazi, Ulezi na Kifo: Ishara za Mwili na Nguvu ya Kujihuisha Miongoni mwa Wazaramo*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Wa Mutiso, K. (2012). Motifu ya Hirizi katika Ushairi wa Kiswahili, *Mulika*, 31: 115-135.

_______(2015). Dhana na Dhima ya Nambari Tatu katika Utendi wa Ayubu, *Kioo cha Lugha*. 13:50-67.